**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – (SBAU) MHE. JENISTA MHAGAMA (MB) WAKATI AKIMKARIBISHA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE. DKT. ALLY MOHAMED SHEIN KUFUNGUA MKUTANO WA KWANZA WA KAMATI YA MAWAZIRI WENYE DHAMANA YA MENEJIMENTI YA MAAFA KWA NCHI WANACHAMA WA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA**
**HOTELI YA MADNAT AL BAHR, ZANZIBAR**
**TAREHE 21 FEBRUARI, 2020**

**Ndugu Mgeni Rasmi, Mhe Dk. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;**
**Waheshimiwa Mawaziri wenye dhamana ya Menejimenti ya Maafa kutoka nchini wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;**

**Mheshimiwa Dkt. Stagomena Tax, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;**

**Makatibu Wakuu wa Sekta mbalimbali;**

**Mheshimiwa Dkt. Thembinkosi Mhlongo, Naibu Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;**

**Wakurugenzi na Maofisa mbalimbali Waandamizi;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana;**

RASIMU

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Awali ya yote, naomba kumshukuru mwenyezi mungu kwa kuweza kutujalia afya njema na kutuwezesha kuandaa na kuhudhuria katika Mkutano huu muhimu wa viongozi wanaoshughulikia masuala ya maafa kwa nchi za SADC unaofanyika kwa mara ya kwanza hapa visiwani Zanzibar. Naomba kuchukua fursa hii kuwakaribisha wote katika mkutano huu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Serikali ya Tanzania inakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kwanza wa Kamati ya Mawaziri wanaohusika na Menejimenti ya Maafa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika baada ya Tanzania kuchukua rasmi nafasi ya Mwenyekiti wa jumuiya kuanzia mwezi Agosti, 2019 kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mwezi Agosti, mwaka huu (2020). Hatua hii inatokana na utaratibu wa kawaida wa mzunguko wa kushika nafasi hiyo kulingana na mkataba wa kuanzishwa kwa jumuiya hii ya SADC.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kama tunavyofahamu, mkutano huu unafanyika kwa mara ya kwanza chini ya uenyekiti wa Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu akabidhiwe uenyekiti wa jumuiya hii. Kufanyika kwa mkutano huu ni fursa kubwa kwa wananchi wa Tanzania kwani utasaidia kukuza biashara na utalii katika nchi yetu hususan visiwa vya Zanzibar na kuendelea kujitangaza kimataifa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kamati ya Mawaziri wenye dhamana ya Menejimenti ya Maafa ilianzishwa kwa lengo la kulishauri Baraza la Mawaziri wa nchi za jumuiya kuhusu masuala ya upunguzaji wa madhara ya maafa kikanda. Malengo mengine mahsusi ya Kamati hii ya Mawaziri ni pamoja na: Kujadili na kuridhia makubaliano ya kikanda na kimataifa; Kutoa maelekezo ya kimkakati na kuisimamia Sekretarieti ya Jumuiya na Nchi Wanachama katika kutekeleza kwa ufanisi shughuli za mzingo wa usimamizi wa maafa ambao umejikita katika Kuzuia, Kupunguza madhara, Kujiandaa, Kukabili na Kurejesha hali. Kamati hii pia itawasilisha hoja katika Baraza kwa ajili ya maridhiano; na inalenga kuwa na jukwaa kwa ajili ya kubadilishana taarifa, uzoefu wa kiutendaji na mbinu pamoja na kujifunza miongoni mwa nchi wanachama.

RASIMU

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mkutano huu unakuja katika kipindi ambacho nchi nyingi wanachama wa ukanda huu zimekuwa zikiathiriwa na majanga ya asili mara kwa mara na kusababisha madhara makubwa. Sote tunakumbuka madahara makubwa ya ukame yaliyotokea mnamo mwaka 2016 ambao uliathiri takribani watu milioni 40 katika ukanda wa SADC na kusababisha ukosefu mkubwa wa chakula. Idadi hii iliongezeka hadi watu milioni 41.6 katika nchi 16 Wanachama katika kipindi cha msimu wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwanzoni mwa mwaka 2019 nchi kadhaa (Komoro, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe) zilipata mafuriko yaliyosababishwa na Vimbunga Idai na Kenneth. Gharama za misaada ya kukabiliana na madhara zilikadiriwa kuwa dola milioni 323, wakati gharama za kurejesha hali zilikadiriwa kuwa dola bilioni 10. Hii inaonesha kuwa gharama za kushughulikia maafa haya pamoja na madhara ya ukame, mafuriko na madhara mengine hulazimisha Nchi Wanachama kuelekeza rasilimali za maendeleo katika misaada na kurejesha hali. Kutokana na Vimbunga vya Idai na Keneth, Nchi yetu pia ilishiriki kutoa misaada mbalimbali ya kibinadamu ikiwemo tani 24 za dawa za binadamu na mahindi tani 200 kwa nchi 3 zilizoathirika zaidi ambazo ni Msumbiji, Malawi na Zimbabwe.

Kwa upande mwingine, magonjwa ya mlipuko yamekuwa yakitokea kwa wanyama na mazao, katika ukanda huu ambao asilimia kubwa ya wananchi wake hutegemea sana shughuli za kilimo kwa ustawi wa uchumi. Hali hii imekuwa ikichangia kudumaza ukuaji wa uchumi wa kikanda.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ukitazama aina ya majanga yanayotokea mara kwa mara, inadhihirisha umuhimu wa ushirikiano wa kikanda ulio thabiti katika kukabiliana nayo. Majanga haya kwa kiasi kikubwa yanatokana na mabadiliko ya tabianchi na hali mbaya ya hewa, masuala ambayo hayana mipaka. Hivyo, hatuna budi kuchukua hatua kwa pamoja za kupunguza madhara na kuimarisha utayari wa kikanda na uwezo wa kukabiliana na maafa.

RASMI

Katika kuchukua hatua za kuimarisha ustahimilivu wa kikanda dhidi ya maafa, Sekretarieti ya Jumuiya kwa kushirikiana na nchi wanachama imekuwa ikichukua juhudi mbalimbali ikiwemo kuandaa Mpango wa Dharura wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa; kushirikiana kuandaa taarifa za utabiri wa msimu na kutoa tahadhari ya awali kuhusu hatari zitokanazo hali ya hewa; na kutoa mafunzo kwa wataalam wa nchi wanachama katika fani mbalimbali ikiwemo tathmini, utafutaji na uokoaji. Aidha, baadhi ya nchi wanachama ikiwemo Tanzania zimefaidika kwa kupata vifaa na mifumo ya kufuatilia majanga ya mafuriko, ukame na moto wa misituni kwa ajili ya kutoa tahadhari ya awali.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ili kwenda sambamba na juhudi za kikanda na kimataifa, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Rais Dk.John Pombe Joseph Magufuli itaendelea kuimarisha uwezo wake wa usimamizi wa maafa katika nyanja zote. Hatua ambazo zimechukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Taifa Kupunguza Madhara ya Maafa; kuandaa Wasifu wa Janga la Mafuriko na Ukame; kuandaa Mpango wa Dhamira ya Taifa wa Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi; kuandaa Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji wa Taarifa za Gesi Joto; Kuandaa Mipango ya Kukabiliana na Dharura za Afya ya Binadamu, Mifugo na Wanyama; kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Mazao baada ya Kuvuna n.k.,. Lengo kubwa la serikali ni kuhakikisha kila sekta inazingatia hatua za upunguzaji wa madhara ya maafa katika mipango ya maendeleo na uandaaji wa bajeti ili kupunguza madhara katika jamii na hasara za kiuchumi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mkutano huu wa Kwanza wa Kamati ya Mawaziri wanaohusika na Menejimenti ya Maafa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika utachochea juhudi zilizopo katika kupunguza madhara ya maafa kwa Kujadili na kupitisha Mkakati wa Kujiandaa na Kukabilina na Maafa wa Kikanda 2016 – 2030 na Kujadili na kuridhia Mfumo Mkakati



RASMU

wa Ustahimilivu wa Kikanda 2020 – 2025 ambayo itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa Mkakati wa Sendai wa Kupunguza Madhara ya Maafa 2025 – 2030 na Mkakati wa Afrika wa Kupunguza Madhara ya Maafa pamoja na Programu yake ya Utekelezaji wa Mkakati wa Sendai kwa Afrika. Vilevile, mkutano huu utapitia maombi ya nchi wanachama kuunga mkono Sekretarieti ya Jumuiya kupata idhini ya matumizi ya Mfuko wa Fedha za Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabianchi na Kupokea taarifa za maendeleo juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango Kazi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwisho, mkutano huu pia utapokea taarifa ya hatua za utekelezaji wa maazimio mbalimbali ikiwemo kuanzisha Mfuko wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Kikanda; kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Operesheni ya Maafa; Mpango wa Mazoezi ya Nadharia ya Kukabiliana na Dharura; pendekezo la Mfumo wa Ushirikiano wa Rasilimali ikiwemo wataalam, fedha na vifaa wakati wa dharura; na Utafiti wa Njia Mbadala za Ufadhili wa Majanga katika huduma za kibinadamu na urejeshaji wa miundombinu kutokana na majanga ya asili.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya kusema hayo machache, naomba sasa nitumie fursa hii kukurabibisha ili uweze kuzungumza na wajumbe wa Kamati ya Mawaziri wanaohusika na Menejimenti ya Maafa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na kutufungulia rasmi mkutano huu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Karibu!**